16. Quiet American

16. Quiet American

Karibu kwenye muhtasari wa kitabu cha KUMI NA SITA kwenye orodha ya vitabu 100 ninavyosoma kwa siku 100.
Quiet American ni riwaya iliyoandikwa na Graham Greene inayohusu vita ya Vietnam na urafiki uliojengeka na kuishia kwenye mauaji.

👉1
Fowlair anamsubiria Pyle kwenye chumba chake ambaye alimwambia atakuja saa nne usiku kwa sababu ana jambo muhimu wanataka waongee.
Fowlair ni Mwingereza, mwandishi wa habari na Pyle ni Mmarekani afisa wa taasisi ya serikali, wote wako nchini Vietnam wakati wa vita.
Saa nne imefika na Pyle hajafika, Fowlair anashangazwa maana Pyle hana tabia ya kuchelewa.
Anatoka nje na kukutana na Phuong mwanamke wa Vietnam ambaye ana mahusiano na Pyle, anamwambia anamsubiri hapo nje, Fowlair anamwambia siyo sehemu salama, aingie ndani.
Wanaingia ndani, Phuong anatengeneza chai na kisha kumtengenezea Fowlair kiko cha kuvuta, huku Fowlair akiwa amejilaza kitandani.
Wanaongea kuhusu Pyle, Phuong anasema ameahidi atamuoa, Fowlair anaitikia.
Hawana mengi ya kuongea maana Phuong hajui sana kiingereza wala kifaransa, anajiuliza wakiwa na Pyle huwa wanazungumza nini.
Fowlair ameshavuta kiko mbili, yuko ya tatu, anajiambia kwa muda huo Pyle hawezi kuja tena, hivyo itabidi huyo mwanamke alale hapo.
Ghafla wanasikia mlango unagongwa, wanafungua na kukuta ni polisi, anamwambia wanahitija kituo cha polisi muda huo.
Wanaenda na wanahojiwa, Fowlair anaulizwa anamfahamu vipi Pyle, anajibu ni Mmarekani, miaka 32 na alifanya kazi kwenye shirika la misaada ya kiuchumi.
Anamuuliza kama walikuwa marafiki, anamjibu ndiyo, walijuana tangu anakuja Vietnam na wamekuwa karibu, anamuelezea kama mtu mpole.
Polisi anamuuliza vipi kuhusu mahusiano yao na Phuong, ambaye awali alikuwa akiishi naye, ila baadaye akaenda kuishi na Pyle.
Fowlair anajibu ni kweli alikuwa anaishi na Phuong lakini baadaye mwanamke huyo akavutiwa zaidi na Pyle ambaye aliahidi kumuoa na hajawa na wivu kuhusu hilo.
Fowlair anagundua Pyle atakuwa ameuawa, anawauliza polisi ameuawa wapi na saa ngapi, wanamweleza.
Wanamtaka aeleze alikuwa wapi kati ya saa 12 jioni mpaka saa 4 usiku, anaeleza maeneo yote.
Wanampeleka ulipo mwili wa Pyle, anaoneshwa, umepigwa risasi kifuani na ukazamishwa kwenye matope.
Polisi wanamwambia Pyle alikuwa na maovu mengi, kabla ya kifo chake amesababisha vifo vya zaidi ya watu 50.
Mahojiano yanakamilika, anaondoka na kurudi nyumbani akiambatana na Phuong ambaye bado hajui kilichotokea.
Wanafika nyumbani, Phuong anamtengenezea Fowlair kiko nyingine na hapo Fowlair anamweleza kwamba Pyle ameuawa.
Phuong anapigwa na butwaa na kukaa kimya kwa muda, kisha baadaye anaendelea kutengeneza kiko.
Fowlair anaona jinsi ambavyo Phuong alimuacha na kwenda kwa Pyle kwa kuwa alikuwa kijana zaidi na kumuahidi kumuoa, na sasa ndoto zote zimeyeyuka.

Anavuta kiko yake na wanalala pamoja, anafikiria kwa muda mrefu amekuwa akilala mpweke, pia anaona huenda ni yeye tu aliyejali sana kuhusu Pyle.

👉2
Fowlair anakumbuka jinsi alivyokutana na na Pyle siku za mwanzo wakati anakuja Vietnam. Hakuwa mtu anayeongea sana, alionekana kuwa amesoma vitabu vingi kabla ya kufika Vietnam.
Moja ya vitabu hivyo ni kinachoitwa The Advance of Red China, kilichoandikwa na York Harding.
Anamwomba Fowlair amfafanulie na kumwonesha yale yaliyoelezwa kwenye kitabu.
Anamweleza jinsi maeneo hayo yalivyo na jinsi vita inavyoendelea. Anamwelezea kuhusu pande mbalimbali zinazopigana kwenye vita hiyo na maeneo ambayo pande hizo zinadhibiti.
Pyle anamshawishi sana Fowlair asome vitabu vya York Harding, kitu ambacho Fowlair hajali sana.

Siku inayofuata wanaamka na hakuna anayemuongelea Pyle.
Fowlair anajiambia maisha yake ya awali yamerudi, anamuuliza Phuong kama atalala hapo siku hiyo, anamjibu inabidi akachukue vitu vyake alikokuwa anakaa Pyle.
Fowlair anamjibu polisi watakuwepo hivyo hawatamruhusu kuingia, anaongozana naye, polisi wanamzuia Phuong ila Fowlair anaweza kuingia.
Anaingia ndani kwa Pyle na kumkuta mkuu wa polisi aliyemhoji akiwa ndani. Anachukua begi la Phuong na kuweka nguo zake, katika kabati la vitabu vya Pyle anachukua kitabu kinachoitwa The Role of the West kilichoandikwa na York Harding.
Polisi anamuuliza kama amepata taarifa zaidi kuhusu mauaji ya Pyle, Fowlair anajibu yanasemwa mengi, hivyo bado kuna utata wa nani kahusika.
Fowlair anamuuliza polisi kama wanafanya uchunguzi zaidi kwenye hilo, polisi anamjibu anaandika tu ripoti, hakuna mwenye muda wa uchunguzi wa kifo kimoja kimoja wakati wa vita
Fowlair anakutana na mkuu wa kitengo cha misaada ya kiuchumi ambacho ndiyo Pyle alikuwa anafanya kazi. Mkuu huyo anaelezea jinsi alivyosikitishwa na kifo cha Pyle na kwamba yeye na baba yake Pyle wanajuana.
Anaeleza alivyotuma taarifa ya kifo chake Marekani na jinsi ubalozi unavyolifanyia hilo kazi.
Mkuu huyo anamuuliza Fowlair kama anaweza kujua kwa nini Pyle ameuawa na nani kamuua. Swali hilo linamkasirisha na kujikuta akisema Pyle ameuawa kwa sababu alikuwa mtoto na mjinga, akijihusisha na mambo yasiyomhusu. Alikuja Vietnam akiwa amesoma vitabu vingi na kufikiri uhalisia ni rahisi kama inavyoelezea kwenye vitabu, mwishowe ameishia kuuawa.
Mkuu yule anamwambia alidhani walikuwa marafiki hivyo angemuongelea vizuri. Fowlair anamjibu ndiyo walikuwa marafiki, lakini angependa kumuona akihangaika na yale yanayomhusu.
Mkuu yule anampa pole kwa kilichotokea kwa Phuong, kwa Pyle kumchukua kwake.
Fowlair na Phuong wanaondoka.

👉3
Fowlair anajikumbusha siku ya kwanza Pyle kukutana na Phuong. Walikuwa na Phuong sehemu ya starehe wakipata kinywaji, Pyle akaja na kuwasalimia, Fowlair akawatambulisha.
Pyle akawaomba wahamie kwenye meza yao, ambapo alikuwa amekaa na Mmarekani mwenzake ambaye wanafanya kazi kwenye shurika moja.
Fowlair anakubali na wanahamia pale, wanaendelea kuongea kuhusu vita inayoendelea.
Ghafla anakuja mwandishi mmarekani anayeonekana amelewa na kujiunga nao. Anaitwa Granger, anamuona Phuong na kumuuliza Pyle amemtoa wapi mwanamke mzuri hivyo, anamtaka awe na tahadhari. Pyle anamuomba Fowlair samahani kwa hayo, hakutegemea mtu huyo angekuja.
Fowlair anamwambia Pyle waende sehemu nyingine tulivu, Granger anasema anaenda sehemu yenye wanawake wanaojiuza na kumtaka Pyle waongozane.
Fowlair anatangulia kwenye klabu nyingine na Phuong, kisha anamuacha akiagiza na kwenda kumfuata Pyle ambaye alijisikia wito wa kumlinda ndani yake.
Kuna wakati alimuuliza Phuong anamuonaje Pyle, akamjibu ni mkimya.
Fowlair anaenda kwenye eneo la wanawake wanaojiuza na kukuta Granger na Pyle wamezungukwa

na wanawake wanaowagombania, anamtoa pale kwa nguvu na kuondoka naye.
Wanakuta Phuong ameshaagiza, wanakula pamoja kisha Pyle na Phuong wanaenda kucheza mziki, Fowlair anabaki amekaa. Pyle siyo mchezaji mzuri ila Phuong anacheza vizuri sana.
Dada yake Phuong anakuja kuongea na Fowlair, mziki unapoisha Pyle na Phuong wanarudi kukaa, anatambulishwa kwa dada wa Phuong.
Wanaongea mengi, dada anaonekana kuvutiwa sana na Pyle, anamweleza jinsi mdogo wake alivyo mrembo kuliko wengine kwenye mji huo, anayependa mtu anayemjali na anayependa sana watoto.
Dada huyo anaondoka na kuwaacha. Pyle na Phuong wanaenda tena kucheza, wanaonekana kujenga ukaribu wa haraka. Wanaporudi Pyle anamuomba Fowlair samahani kwa kucheza na mwanamke wake, Fowlair anamjibu asijali, yeye siyo mchezaji mzuri ila anapenda kuangalia wengine wakicheza.
Wanamaliza na kuondoka.

👉4
Shambulio kubwa limetokea kwenye mji wa Phat Diem, mji umezingirwa na maadui na watu wengi wameuawa.
Fowlair kama ripota ametoka Saigon na kuja eneo la mapambano, lakini kwa kuwa upande wao umeshindwa kwenye shambulio hilo, hakuwa na cha kuandika, maana wao wanaandika kuhusu ushindi tu na siyo kushindwa.
Mji mzima watu wameuawa na waliosalia wamekimbilia kwenye kanisa, ambapo wanaamini ni salama na hawawezi kushambuliwa.
Fowlair anaungana na kundi la jeshi la wafaransa ambalo lilikua linaelekea mji mwingine. Wanavuka mito ambayo inaelea miili ya watu, wanapita njia ambazo pembeni ni maiti.
Hilo linamfanya Fowlair afikirie sana kuhusu maisha na kifo, anaiona miili ile na kuona jinsi imekosa thamani baada ya kifo.
Wanafika nyumba watakayopumzika kwa usiku huo, anapewa sehemu atakayolala na kukabidhiwa bastola. Wanaambiwa walale kidogo na saa sita na nusu usiku wawe macho, maana saa kumi ndiyo mapambano huwa yanaanza.
Analala na kuota Pyle anacheza jukwaani na mtu asiyeonekana, huku yeye akimwangalia na kumlinda kwa bastola mtu asimkatishe.
Anashtuka na kuona mtu amesimama ameshika mshumaa, kumwangalia ni Pyle.
Anashangazwa amefikaje hapo, Pyle anamweleza jinsi alivyopita maeneo ya hatari mpaka kufika hapo.
Anamuuliza nini kimemleta, anamwambia alitaka sana kufika eneo la mapambano, ila anamwambia nia hasa ni alitaka kuongea naye.
Pyle anamwambia Fowlair kwamba amempenda sana Phuong na ameona amwambie yeye kwanza kabla hajaongea na Phuong.
Fowlair anacheka sana, anamwambia kwa nini asingesubiri mpaka arudi? Pyle akamjibu alihofia anaweza kufa kwenye vita hiyo halafu akajisikia vibaya kuwa na Phuong wakati hakumwambia.
Pyle anamwambia Fowlair atakachofanya ni kumwambia Phuong kwamba anampenda na yupo tayari kumuoa, kisha achague mwenyewe, kama atabaki ba Fowlair au atamuacha na kwenda kwake.
Fowlair anamuuliza vipi kama Phuong atamkataa, Pyle anajibu ataomba kuhamishwa kituo cha kazi.
Fowlair anamwambia kwa nini asiondoke tu kabla hajaleta mvurugano? Pyle anamjibu Fowlair kwamba hajamuelewa vizuri Phuong na ndiyo maana hana furaha.
Anamuuliza kipi alichomuelewa, anamwambia Phuong anapenda watoto ila yeye Fowlair hawezi kumpatia.
Fowlair anamwambia amedanganyika na maneno ya dada yake Phuong, yule anachoangalia ni pesa tu, anajua Pyle atakuwa na pesa kuliko yeye na hivyo kutafuta njia ya kumteka.
Pia anamwambia yeye tayari ana mke nyumbani, hivyl hawezi kumuoa Phuong ila wana furaha pamoja hivyo ni bora asiingilie.
Pyle anamwambia Fowlair anashukuru amemuelewa kwenye hilo na sasa ana amani. Ataenda kumwambia Phuong ili achague mwenyewe.

Siku nyingi baadaye Fowlair anakumbuka tukio hilo na kujiuliza nani aliyemuelewa zaidi Phuong, Pyle aliyekufa au yeye Fowlair ambaye amelala naye sasa.

👉5
Asubuhi inayofuata Fowlair anaamka na kukuta Pyle ameshaondoka, yeye inamchukua wiki nzima mpaka kuja kuondoka kwani njia zimefungwa.
Anakuja kugundua Pyle aliweza kuwashawishi wanajeshi wanaofanya ulinzi kwa ndege wakambeba kutoka mji huo mpaka mji mwingine wa Hanoi.
Fowlair anapofika Hanoi anakuta Pyle amemuachia barua, akimshukuru kwa namna alivyomsikiliza kwani sasa anajiona siyo mtu mbaya tena.
Anamwambia asiwe na wasiwasi kwa yeye kutangulia kuondoka, kwani hataongea na Phuong mpaka yeye Fowlair arudi.
Fowlair anahudhuria mkutano wa mkuu wa kikosi cha jeshi la Ufaransa na waandishi wa habari, anaeleza kwamba wameweza kuwashinda maadui na sasa wanakimbia.
Fowlair hasikilizi kwa umakini, muda mwingi anafikiria kile Pyle amemwambia huku akiona Phuong akimuacha, kwani anajua kwenye ushindani wa kimapenzi, ujana na pesa vina nguvu kubwa, vitu viwili ambavyo Pyle anavyo ila yeye hana.
Fowlair anapokea taarifa kwamba amepandishwa cheo kutoka kuwa ripota mpaka kuwa mhariri na hivyo anapaswa kurudi London ambapo ndipo atafanyia kazi yake.
Hafurahii hilo, anajiambia kazi ya uripota siyo ngumu, unaeleza kile kilichotokea, lakini uhariri ni mgumu kwa kuwa unatakiwa kuandika maoni yako.

👉6
Fowlair amerudi Saigon na anaandika barua ya kuomba abaki na kazi yake, anaeleza anafurahia kwa sasa na kama atalazimika kuchukua nafasi hiyo nyingine basi yuko tayari kuacha kazi.
Anamuomba sana mhariri mkuu amuache huko huko Vietnam kwa sababu pia huo siyo wakati mzuri wa kubadili ripota.
Pyle alikuwa amemuahidi atakuja kwake, Phuong anasema anaenda kwa dada yake.
Pyle anafika na kumkuta Fowlair mwenyewe, anamwambia ni mara ya mwanza wanakutana tangu walioongea mara ya mwisho.
Fowlair alikuwa anafikiri kilichotokea ni utani tu, japo barua aliyomuachia alikuwa nayo. Ila sasa alipomkumbusha ndiyo akaona kweli alimaanisha.
Pyle anamwambia amekuja wamalizie mazungumzo kuhusu Phuong, Fowlair anamwambia ametoka.
Wanazungumza kuhusu taarifa zinazosambaa kwamba vifurishi vya misaada ya Wamarekani vimekutwa na plastiki. Pyle anajitetea kwamba siyo kwa nia mbaya, wanataka kusaidia uchumi wa hapo ukue.
Wakiwa hapo Phuong anakuja, Pyle anamweleza Fowlair kwamba huo ndiyo wakati mzuri wa kuweka mambo wazi ili Phuong achague mwenyewe.
Changamoto ni Phuong haelewi vizuri Kiingereza na Pyle haelewi vizuri Kifaransa hacha cha lafudhi ya Vietnam.
Pyle anamuomba Fowlair awe mkalimani wa kuwatafsiria. Fowlair anashangazwa ila anakubali.
Pyle anaeleza jinsi anavyompenda Phuong na alivyo tayari kumuoa ili ampe maisha mazuri na ya heshima.
Fowlair anatafsiri kila kitu kama anavyosema Pyle, Phuong anashtushwa na kuuliza kama ni utani au kweli.
Anajibiwa ni kweli. Pyle anamuuliza Phuong kama yupo tayari, anajibu hapana.
Pyle anahuzunishwa na jibu hilo na kujibu sawa, anamuomba Fowlair samahani kwa hayo aliyosababisha na kuahidi kutokuwasumbua tena na anaondoka zake.
Phuong anamtengenezea Fowlair kiko huku Fowlair akiandika barua nyingine, hii sasa anamwandikia mke wake, anamwambia anarudi London, anamshukuru kwa miaka ambayo wamekuwa pamoja, japo walikuwa hawaishi kugombana. Anamuomba ampe talaka kwa sababu anaona hawawezi tena

kuendelea pamoja. Anamwambia tangu wameoana wamekuwa wanaambiana ukweli na sasa anamweleza ana mwanamke mwingine ambaye anampenda sana na hayupo tayari kumuacha, amepanga kumuoa.
Baada ya kumaliza kuandika barua anaenda alipo Phuong na kuanza kuvuta kiko. Anamweleza kuhusu safari ya kurudi London, Phuong anashtushwa na kumwambia anajua hataenda, Fowlair anamjibu hajajua.
Phuong anamwambia yuko tayari kwenda naye London, Fowlair anamjibu itakuwa ngumu, japo ameshamuandikia mke wake barua ya kumuomba talaka.
Phuong anamwambia ataenda naye hata iweje. Anamuuliza jinsi London ilivyo, iwapo kuna maghorofa na kama ataona yale amekuwa anaona kwenye sinema.
Fowlair anamjibu kama anataka kuona mengi ya kwenye sinema inabidi aende Marekani.

👉7
Fowlair ameenda kwenye sherehe ya dini inayoitwa Caodaism, hiyo ni dini ambayo imechanganya ukristo, ubudha na uconfusian kwa pamoja.
Huwa wana sherehe kubwa zinazofanyika kila mwaka na kuhudhuriwa na wengi, wengi huhudhuria siyo kama waumini, bali kwenda kujionea mambo mbalimbali.
Fowlair anapata nafasi ya kumhoji msaidizi wa papa wa dini hiyo, ambaye anamweleza misingi ya dini yao.
Fowlair anakutana na Pyle ambaye pia alikuja kwenye sherehe hizo, ila gari yake imeharibika, anamwambia amuombe mmoja wa wanajeshi akatafute fundi.
Sherehe inaisha na wanataka kuondoka, lakini bado fundi hajafika, wanapaswa kuondoka mapema maana kuna masharti ya mwisho kutembea barabarani ni saa moja usiku.
Fowlair anamwambia Pyle atampa lifti kwenye gari yake waende, gari ikiwa tayari itumwe kesho yake.
Wanapanda gari na kuondoka, katikati ya safari gari imeisha mafuta, Fowlair anasema alijaza tenki, itakuwa wahuni wameiba mafuta kwenye gari hiyo.
Wanaona mnara mbele, wanapaki gari na kwenda kwenye mnara huo, wanakuta wanajeshi wawili wa kivietnam wameshika bunduki.
Fowlair anawaambia wao siyo watu wabaya, wanaomba hifadhi mpaka pakuche waendelee na safari.
Watu hao hawawajibu kitu, lakini pia hawaoneshi kutaka kuwadhuru.
Hivyo Fowlair na Pyle wanakaa na kuanza kuongea, wanaongea mengi kuhusu mapenzi, dini na siasa.
Kwenye mapenzi Pyle bado anaonekana kumpenda Phuong na anamuuliza Fowlair kama anampenda kweli. Anamjibu kwa umri wake anahitaji sana mwanamke ambaye anaweza kuwa naye karibu ili asimalize maisha yake kwa upweke.
Kwenye siasa Fowlair anaeleza jinsi vita hiyo ya Vietnam isivyo na mantiki, kwani wametoka mbali kuja kuvuruga maisha ya wavietnam kwa kisingizio cha demokrasia na soko huria. Anasema wavietnam wengi hawajali vitu hivyo, wanachojali ni waweze kulima mpunga na kuuza mwa wengine ili kupata mahitaji yao.
Kwenye dini Pyle anamuuliza Fowlair kama anaamini kwenye uwepo wa Mungu, anajibu hapana. Anawambia lazima awe kuna kitu anaamini, hakuna binadamu anaweza kuishi bila imani. Fowlair anamjibu anaamini mengi, yale yanayoonekana na siyo yasiyoonekana.
Wakiwa kwenye mnara huo wanasikia sauti inaita kwa kipaza sauti, inatumia lugha ya Vietnam hivyo hawaelewi.
Wanajaribu kuwauliza wanajeshi wale sauti inaashiria nini hawajibu. Sauti inarudia tena na tena, Fowlair anamwambia Pyle kwamba wavietnam watakuwa wameona gari lao na hivyo wanawataka wanajeshi hao wawasalimishe la sivyo watashambulia.
Anamwambia waondoke haraka kwenye mnara huo, wanafanya hivyo, ila Fowlair anaanguka na kuvunjika mguu.
Hawezi kutembea, anamtaka Pyle aondoke na kumwacha, maana hatari ni kubwa. Pyle anamjibu hatomuacha, anamsaidia kwa upande wa mguu uliovunjika na wanasogea mpaka kwenye shamba la mpunga.

Mnara ule unalipuliwa na kuharibiwa kabisa, gari inachomwa moto.
Wanajificha kwa muda, wanasikia risasi zinapigwa kisha kunatulia. Pyle anamwambia Fowlair amsubiri hapo, atasogea barabarani ili gari la wanajeshi wa ulinzi likipita aombe msaada. Fowlair anamwambia hiyo ni hatari, anaweza kupigwa risasi, hamsikilizi, anaondoka.
Fowlair anabaki pale akiugulia maumivu, anafikiria jinsi Pyle alivyomsaidia licha ya kumsisitiza aondoke na kumuacha.
Pyle anarudi na msaada na wanamchukua Fowlair ambaye maumivu yamekuwa makali mpaka anaona kama fahamu zake hazipo vizuri.

👉8
Fowlair ametoka hospitali baada ya kukaa muda mrefu, anatumia magongo kutembea. Anafika nyumbani na kumkuta Phuong amnaye anamwambia amemkosa kwa muda mrefu, anafurahia hilo.
Anamuuliza kama kuna sinema mpya imetoka wakati hayupo, Phuong anaanza kumsimulia. Fowlair hasikilizi kwa umakini, anafikiria kama kuna barua zimetumwa wakati hayupo.
Phuong anamwambia kuna barua za kazi ambazo dada yake amemsaidia kuzisoma ila kuna moja binafsi hajaisoma.
Fowlair anachukua barua hiyo na kuifungua, ni ndefu na jina la mwandishi ni mke wake. Anakaa kuanza kuisoma. Mke wake anamweleza amepokea barua yake na jibu lake ni hapana, hatampa talaka kwa sababu mbili. Moja dini yake hairuhusu na mbili Fowlair ni muongo na tapeli wa mapenzi.
Anamwambia ameandika kwamba amepata mwanamke anayempenda sana na hawezi kuishi bila yeye, hivyo ndivyo alivyomwambia pia na ushahidi wa barua anao, lakini ameishia kumuumiza. Hivyo anamwambia hatampa talaka, maana hiyo itakuwa tiketi ya kwenda kumuumiza mwanamke mwingine.
Phuong anamuuliza kama barua ina habari njema, Fowlair anajibu mke wake amekataa kumpa talaka. Ila anamwambia bado kuna matumaini.
Phuong anamwandalia kiko, anavuta na kisha kuandika barua kwa Pyle ambaye hawajaonana, anamshukuru kwa kumuokoa na kumwambia asijali Phuong yuko salama.
Fowlair anamtembelea rafiki yake waliokuwa wanaripoti pamoja, ambaye kwa sasa anaumwa. Anamwuliza anamjuaje Pyle, Fowlair anajibu wamekuwa wakikutana mara kwa mara.
Rafiki yake anamwambia kuna mpango unaofanywa na Wamarekani ambao siyo mzuri na Pyle anahusika. Anampa anwani akaonane na mchina mwenye godauni kubwa la kuhifadhi vyuma.
Fowlair anaenda pale na kuoneshwa pipa kubwa lililokuwa limebeba kemikali fulani inayohusika na plastiki, lakini hawajui ni plastiki kwa matumizi gani.
Mtu yule anamwambia wamemuonesha yeye maana wanajua hana upande, hivyo wanategemea ataweza kuandika kutahadharisha hilo, ila wanamtaka asitaje kama ameona mapipa ya kemikali.
Fowlair amepumzika nyumbani, anafikiria jinsi ya kukutana na Pyle, anasikia mlango unagongwa, ni Pyle lakini mguu wake unamuuma haendi kufungua. Mara anasikia minong'ono ya chini, anaamua akafungue, anakuta Pyle na Phuong wamesimama pamoja kama walikuwa wanapigana busu.
Fowlair anamkaribisha Pyle ndani na kumuuliza kama alipata barua yake, anajibu ameipata na ni bora asingeiandika.
Pyle anameambia Fowlair hakutegemea ni muongo, anauliza amedanganya nini, anamwambia barua ya mke wake wameiona, Phuong aliipeleka kwa dada yake amsaidie kutafsiri
Pyle analalamika kwa nini Fowlair hakumweleza ukweli Phuong, anamjibu alitaka kumlinda tu, Pyle anamwambia ni uongo, ni mbinafsi.
Fowlair anamwambia Pyle vipi kuhusu mradi wao wa plastiki usioeleweka, Pyle anashangaa kusikia hayo.
Pyle anaamua kuondoka, Fowlair anamwambia nenda tu, nenda katekeleze mradi wako wa plastiki.
Baadaye Fowlair anakumbuka huenda alifuata huo ushauri wake, kwa yake Pyle alikwenda kufanya.

👉9
Wiki mbili baada ya kifo cha Pyle, Fowlair anakutana na polisi aliyemhoji kwenye eneo la starehe.

Wanacheza pamoja mchezo wa kushindana na kuwa na maongezi.
Polisi anamgusia kuhusu kifo cha Pyle, Fowlair anamuuliza kama bado wanakifuatilia, polisi anamjibu kuna afisa wa ubalozi wa Marekani amekuwa anafuatilia sana kifo hicho.
Polisi anamueleza Fowlair kwamba wamempata mbwa wa Pyle ambaye pia aliuawa na wanamfanyia uchunguzi, hasa kwenye miguu yake kujua udongo wa alipotembelea, kama ambavyo Fowlair alishauri wakati anahojiwa.
Polisi anamwambia Fowlair anataka kuwa na maongezi naye ya siri hivyo atamtembelea nyumbani kwake wakati Phuong hayupo.

Tangu Pyle alipoondoka kwa Fowlair hawajaonana tena na mahusiano yane na Phuong yamekuwa siyo mazuri.
Mara kwa mara haonekani na akimuuliza alikuwa wapi anajibu kwa dada yake.
Akimuuliza lini ameonana na Pyle anajibu hajaonana naye.
Fowlair anaona kuna kitu hakipo sawa.
Anapokea ujumbe wa kukutana na yule aliyemueleza kuhusu kemikali za plastiki za wamarekani.
Wanakutana sehemu ya mji yenye baiskeli nyingi na saa tano kamili baiskeli zinaanza kulipuka na kutoa plastiki.
Mtu yule anamuonesha kwamba ile kemikali ilitumika kutengeneza mabomu ya plastiki yanayofanana na pampu za baiskeli.
Fowlair anajilaumu kwa nini hakumuuliza Pyle kuhusu hilo, ila anaona haina madhara, kama ni kitu kinachomuweka 'bize' ili asimsumbue mwanamke wake ni sawa.
Fowlair anajaribu kufuatilia tena kule alikoenda na kukuta plastiki ile, ana wasiwasi hao hao ndiyo wanaotengeneza mabomu hayo, anafika ila hakuti chochote.
Anajiambia huenda watu hao wanashirikiana na General The kutengeneza mabomu hayo ya plastiki.
General The ni mmoja wa pande zinazopigana kwenye vita hiyo na taarifa alizopata ni Pyle pia yuko upande wa General The.
Anarudi nyumbani amechoka, anafika na kukuta Phuong hayupo. Anaangalia kwenye chumba na haoni vitu vyake, anapatwa na maumivu makali, Phuong ndiyo ameondoka na kumuacha.
Siku inayofuata anaenda kwenye ofisi anazofanya kazi Pyle na kumuulizia, anaambiwa hajafika ofisini na mara nyingi hufanyia kazi nyumbani.
Bosi wa Pyle anamuuliza Fowlair anataka nini anamjibu Pyle amemchukulia mwanamke wake. Bosi huyo anamwambia hapaswi kumtuhumu hivyo, tena mtu ambaye ameokoa uhai wake.
Fowlair anajibu kwa hasira kwamba hakumtuma amuokoe. Bosi huyo anamwambia hawawezi kuongelea mambo ya mapenzi hapo ofisini.
Anamwambia anaondoka, ila wampe Pyle ujumbe kwamba anamtafuta. Anaingia kwenye choo na kujikuta analia sana, kitu ambacho hakijawahi kumtokea kwa muda mrefu.
Fowlair anaamua kuondoka kwa muda Saigon na kuelekea kaskazini, anakutana na mwanajeshi wa anga wa Ufaransa ambaye anamwambia kama anataka wanaweza kuongozana.
Fowlair hajawahi kupanda ndege inayofanya mashambulizi, hivyo anajikuta kwenye wakati mgumu kwa namna ndege hiyo inavyoendeshwa na kufanya mashambulizi. Muda wote anakuwa na hofu kubwa, lakini anashukuru kwani katika wakati huo hakuwa anamfikiria Phuong au Pyle.
Fowlair anamwambia kapteni yule kwa uharibifu huo alioona, ndiyo maana anachukia sana vita na hana upande wowote kwenye vita hiyo.
Kapteni anamjibu hata wao wanajeshi siyo kwamba wanapenda sana vita, ila wanasiasa ndiyo wanawaambia wapigane, wakishapigana na kuuana, wanasiasa wanakuja kupatana kuleta amani ambayo ilikuwepo kabla ya vita.
Kapteni anamwambia Fowlair japo hana upande sasa itafika wakati atakuwa na upande. Fowler anamjibu hana muda mrefu ataondoka. Anamuuliza vipi kuhusu mwanamke aliyenaye, hamjibu.
Anamwambia asimuache, aende naye. Anamjibu hajui kama itawezekana.

👉10
Fowlair anarudi nyumbani na kukuta mlango wake uko wazi, anaingia kwa shauku akidhani Phuong amerudi.
Kuingia anamkuta Pyle, anamuuliza amewezaje kuingia anamjibu alimkuta rafiki yake ameleta barua na kumwomba aingie na kusubiri.
Fowlair anamuuliza amefata nini, Pyle anamjibu alisikia amefika ofisini kumuulizia, hivyo amekuja waongee.
Fowlair anamuuliza Phuong anaendeleaje, anamjibu anaendelea vizuri. Anamuuliza vipi mpango wa kumuoa, anajibu ameona amue atakaporudi naye nyumani kwao Marekani.
Fowlair anamtaka asilazimishe wala kuharakisha, asije akamuumiza Phuong.
Pyle anamwambia sawa na kushukuru jinsi maongezi hayo yalivyokwenda, hakutegemea yangeenda vizuri hivyo.
Fowlair ndani yake ana hasira, alikuwa amejipanga kumkabili Pyle kwa kile alichofanya, lakini anashangaa kila akikutana naye anamuonea huruma, anamuona kama mtu asiye na hatia.
Fowlair anamwambia Pyle kwamba anapanga kuhama hapo kwa sababu kunamkumbusha sana kuhusu Phuong, lakini pia anamtaka amweke Phuong mbali maana hataki kuonana naye, anachotaka ni awe salama.
Fowlair anaenda kutafuta nyumba nyingine, anakutana na Mfaransa anayeondoka na nyumba yake inabaki wazi, anaiangalia ni nzuri lakini pia ina michoro yenye thamani kubwa ndani yake. Fowlair anamuuliza kama anaweza kumwachia nyumba bila michoro hiyo, mtu huyo anakataa, anamwambia lazima alipie vyote. Lakini pia mtu huyo ana vitabu vingi, ila amesema hivyo haviachi, anaondoka navyo maana ndiyo vinampa kampani anapokuwa na upweke.
Fowlair anaondoka kurudi nyumbani, anakwepa njia ambazo huwa anatumia Phuong kwa sababu anajua huo ndiyo muda wake na Phuong huwa havunji ratiba zake.
Anafika kwenye mgahawa na kuona mabinti wawili wa kimarekani wanakula, mmoja anamwambia mwenzake Warren aliwaambia saa tano isiwakute hapo, na inakaribia hivyo waondoke haraka.
Fowlair anawaangalia mabinti hao wakiondoka na haelewi kwa nini wamekuwa na haraka hivyo. Muda siyo mrefu anasikia mlipuko mkubwa, kuangalia ni jengo la pembeni limelipuliwa kwa bomu.
Anataka kukimbia haraka kuingia maana anajua huo ndiyo muda wa Phuong kuwa kwenye jengo hilo kufanya manunuzi ya mahitaji muhimu.
Polisi wanamzuia na kumwambia hapaswi kuingia eneo la tukio. Anamwambia yeye ni mwandishi, anajisashi atoe kitambulisha anajikuta amekisahau.
Akiwa pale anamuona Pyle anakuja, anamwambia watumie kitambulisho chake kuingia wakamuokoe Phuong, Pyle anamjibu hayupo huko ndani.
Fowlair anamwambia anajua ratiba zake, muda huo lazima awe hapo, Pyle anamjibu alimtahadharisha leo asiende hapo. Fowlair anaunganisha matukio, mabinti wa kimarekani walikuwa wametahadharishwa na Phuong pia ametahadharishwa, ina maana wamarekani walijua mpango huo.
Fowlair anamwambia Pyle wamefanya makosa makubwa sana kwenye mlipuko huo, maana umeua raia tu, hasa wanawame na watoto ambao muda huo ndiyo wanafanya manunuzi.
Pyle anamjibu muda huo kulipaswa kuwa na gwaride la jeshi, Fowlair anamwambia gwaride hilo liliahirishwa jana yake. Pyle anasema hakujua, na kama gwaride liliahirishwa mlipuko huo usingepaswa kufanywa.
Fowlair anamwambia Pyle anachofanya ni hatari, anajaribu kutekeleza nadharia za kwenye vitabu vya York Harding za uhitaji wa Nguvu ya tatu kwenye vita hiyo na anamtumia General The kama nguvu ya tatu, hilo litakuwa na madhara makubwa.
Fowlair anamwambia ni bora amchukue Phuong na kurudi Marekani kuliko kuendelea na majaribio yake ambayo yatagharimu maisha ya wengine.
Fowlair anamuacha Pyle na kuondoka zake.

👉11
Fowlair anampa Phuong fedha aende kuangalia sinema ili apate nafasi ya kukutana na polisi kama

walivyoahidiana.
Polisi anafika, anampa kinywaji na wanaanza mazungunzo.
Polisi anamwambia japo hayupo tena kwenye uchunguzi wa mauaji ya Pyle na japo ana uhakika Fowlair hajamuua, ameona taarifa aliyoitoa haikuwa sahihi.
Polisi anaanza kumwelezea taarifa yake kama alivyoitoa kwa kila muda alipokuwa, inaonekana kuna dakika 10 ambazo hakuzielezea. Na hapo polisi anaamini Fowlair alionana na Pyle kabla ya kifo chake, japo siyo yeye aliyemuua.
Fowlair anamuuliza ana ushahidi gani kwenye hilo, polisi anamjibu ni kutoka kwenye miguu ya mbwa wa Pyle, haikuwa na udongo kama alivyoshauri, bali ilikuwa na sementi, hivyo inaonekaba walipita eneo ambalo ujenzi unaendelea.
Fowlair anamwambia polisi hana maelezo ya ziada ya kumpa, polisi anaondoka.
Fowlair anabaki na mawazo, japo anajua maelezo yake yanaenda kufunga jalada, anatamani angemwambia ndiyo alionana na Pyle kabla ya kifo chake.

👉12
Baada ya kumuacha Pyle pale eneo la tukio, Fowlair anaelekea kwenye lile jengo la wachina alikopata taarifa za kemikali walizonazo wamarekani na Pyle kuhusika.
Amafika na kukuta hali iko kama alivyoiacha mara ya mwisho.
Anawaambia anataka kuonana na Mr. Heng anapelekwa alipo ambapo ni chumba cha ndani zaidi.
Heng anamwambia wamesikia kuhusu mlipuko uliotokea ila hawataki kutoka sana kwa kuwa polisi watakuwa wengi.
Anamuuliza Fowlair atachukua hatua gani kuzuia hilo, maana ukweli wote anao na yeye pekee ndiye anayeweza kuzuia mauaji zaidi yasitokee.
Fowlair anamjibu hata akiandika habari ya kuanika ukweli huo, haitapewa nguvu kwa sababu wamarekani wanachukuliwa hawana upande kwenye vita hiyo na hakuna anayetaka tena kusikia habari za General The.
Heng anamwambia wana mpango wa kumzuia Pyle asiendelee na mipango hiyo, ila wanahitaji msaada wa Fowlair katika kukamilisha hilo.
Wanamwambia Fowlair amkaribishe Pyle kwa chakula cha jioni kwenye hoteli iliyo nje kidogo kati ya saa tatu mpaka saa nne usiku, ila iwe siri yeyote asijue.
Kisha wao watakamilisha mpango wao kwenye daraja ambalo Pyle atapita. Wanamwambia ni yeye Fowlair pekee anayeweza kusaidis hilo na kuzuia mauaji zaidi.
Fowlair anayakumbuka maneno ya kapteni kwenye ndege alipomuambia japo anasema hana upande, kuna wakati atajikuta anachukua upande. Akikumbuka maiti alizoona kwenye mlipuko, anaumia sana, anakubali kufanya hivyo.
Anatoka na kumtumia ujumbe Pyle aje nyumbani kwake, anakuja. Pyle anamwambia Fowlair anashukuru sana kumwita licha ya yale yaliyotokea kwa mlipuko, anamwambia ni kwa nia njema ya kujenga demokrasia, kwani wamarekani wakimsaidia General The akashika madaraka, wanaweza kumdhibiti vizuri akaondoa ukomunisti na kujenga demokrasia.
Fowlair anamwambia mambo siyo rahisi hivyo, kwenye siasa na vita huwa hakuna shukrani, mtu akishapata madaraka hubadilika
Fowlair anajaribu kuzuia hisia zake na kitokuongea sana, Pyle anaongea mengi kuhusu maisha yale jinsi alivyokuzwa na wazazi wake na kuhusu juhudi zake hapo.
Fowlair anamwambia wawe na chakula cha jioni pamoja siku hiyo, Pyle anakubali na kufurahi sana, akisema pamoja na yote, bado urafiki wao unakuwa imara.
Kadiri anavyomsikiliza Pyle, Fowlair anaingiwa na huruma na kutamani kumtahadharisha na hatari iliyo mbele yake. Anamwambia labda waahirishe chakula hicho cha jioni, Pyle anakataa, anasema ni muhimu wawe na chakula hicho pamoja.
Fowlair anamuaga na kumwambia wakutane muda huo, na kama mpaka saa nne usiku watakuwa hawajakutana basi aje hapo nyumbani.
Pyle anaondoka, Fowlair anaenda kumtembelea rafiki mwingine na kufanya naye mazungumzo,

anatoka na kwenda kuangalia sinena kisha saa tatu anaenda walipopanga kukutana. Yote hayo alikuwa anafanya kutengeneza sababu za kujitetea iwapo itahitajika hivyo baadaye.
Saa tatu anafika kwenye hoteli ile, anaambiwa Granger ana sherehe hapo, yeye anasema hajaja kwenye sherehe, hivyo apewe meza ya mtu mmoja. Ni kama alishategemea kwamba Pyle hatafika, hivyo kuwa na sababu zaidi anamsisitizia mhudumu anataka meza ya mtu mmoja, ili kumaanisha hana miadi ya kukutana na yeyote usiku huo.
Mpaka saa nne kamili Pyle hajafika, Granger anamuona Fowlair na kuja kumsalimia. Anamwomba watoke nje ana maongezi naye.
Granger anamweleza wazi Fowlair kwamba hampendi, ila ni yeye pekee anayeweza kumweleza yaliyo moyoni. Anamwambia aliandaa sherehe hiyo kwa sababu ni kumbukizi ya kuzaliwa ya mtoto wake, ila amepata taarifa kwamba mtoto huyo amepata polio.
Anasema kama angekuwa na nafasi ya kuchagua, ni bora angekufa yeye na siyo mtoto.
Fowlair anamfariji kisha baadaye Granger anarudi ndani na Fowlair kurudi nyumbani.
Anafika nyumbani saa nne, hakuna mtu, anasubiri mpaka saa sita, Pyle haji, anaamua kutoka nje ndiyo anakutana na Phuong.

👉13
Phuong anarudi kutoka kwenye sinema na kumuuliza Fowlair kama polisi alikuja, anamjibu ndiyo. Anamuuliza alitaka nini, anamjibu kuna maswali alikuwa anauliza, ila anaamini kwa sasa hatamsumbua tena.
Fowlair anamwambia Phuong amsimulie sinema aliyoangalia, anamwambia haikuwa na mwisho mzuri, kwani walimuua mwanamke kwa kumkata kichwa.
Fowlair anachukua barua na kuzisoma, moja inatoka kwa mke wake ambaye anamwambia ameamua aanze mchakato wa talaka. Anamweleza Phuong ambaye anafurahia sana habari hiyo, anasema ataenda kumwambia dada yake kwamba kuanzia sasa yeye ni Mrs Fowlair.
Fowlair anamuuliza kama huwa anamkumbuka Pyle, hajibu chochote, anamwambia alikuwa kijana, wangefanya mengi pamoja, anamjibu hata yeye wanaweza kufanya mengi pamoja.
Phuong anaondoka kwenda kwa dada yake na kumuacha Fowlair akiwa na majuto, anajiona ni yeye pekee aliyejali kuhusu Pyle.
Miaka mingi baadaye Fowlair anakumbuka haya, anaona japo hatua alizochukua zilizuia mauaji zaidi, lakini bado ndani yake alijiona ana hatia na alitamani apate nafasi ya kuomba msamaha.

👉SOMO
Riwaya hii inatuonesha mikasa mingi ya maisha kwa pamoja, kuanzia vita, urafiki, mapenzi na usaliti. Kuna mengi ya kujifunza tunayoweza kuyatumia kwenye maisha yetu.
1. Tunapaswa kuwa makini na nadharia tunazojifunza kwenye vitabu, nyingi huwa nzuri kwenye maandishi, lakini kwenye uhalisia huwa hazifanyi kazi. Tumeona hilo kwa Pyle ambaye alibeba nadharis za vitabuni na kwenda kuzijaribu na kuishia kusababisha vifo vya wasio na hatia.
Siyo kwenye vita tu hili lina madhara, tunaona kila siku kwenye biashara na uwekezaji watu wanavyopoteza fedha kwa kuamini nadharia ambazo siyo sahihi. Kila nadharia unayojifunza, angalia kwanza uhalisia na pata uzoefu wa walio kwenye utendaji ili uweze kufanya kilicho sahihi.
2. Ni vigumu kutokuwa na upande, kama kweli unajali na unataka kusimama kwenye ukweli, itafika mahali itakubidi uchague upande. Na hata kama hutachagua upande, maana yake tayari umejiweka upande wa wa wakandamizaji. Tumeona jinsi Fowlair alivyokuwa hana upande kwenye vita, lakini ilipofika hatua kwamba yeye tu ndiye anayeweza kuzuia mauaji, ilibidi achague upande, maana asingechagua, angekuwa amekubali mauaji yaendelee.
3. Tunapaswa kuwa wakweli kwa marafiki zetu na kuwaeleza ukweli hata kama utawauma, badala ya kuwaambia yale tu wanayofurahia. Kwa kipindi kirefu Fowlair alitaka sana kumkabili Pyle kuhusu mienendo yake, lakini hakutaka kumuumiza, kitu kilichofanya Pyle aendelee kufanya uharibifu mkubwa.
4. Tumeona jinsi vita zilivyo na madhara makubwa, mauaji ya watu, kuvuruga maisha na huku

matokeo yake yakiwa hayana tija. Kwani mwisho wa vita ni wanasiasa kukubaliana kurejesha amani, ambayo ilikuwepo kabla ya vita.
5. Tumejifunza pia propaganda zinazofanywa na vyombo vya habari hasa nyakati za vita. Vyombo hivyo hutangaza habari za ushindi tu kwa upande wao na siyo za kushindwa.
6. Tumejifunza pia kuwa na utayari wa kufanya maamuzi magumu, ambayo yanaweza kukatisha uhai wa mtu mmoja, lakini ukaokoa uhai wa walio wengi zaidi, hasa pale inapokuwa hakuna namna nyingine.
Japo hakuna kifo kinachoweza kuhalalishwa, lakini maisha huwa hayaendi vile tunavyopanga au kutaka sisi, nyakati za kufanya maamuzi magumu huwa zinatujia na tunapaswa kujua namna ya kufanya maamuzi hayo.

Muhtasari huu umeandaliwa na Kocha Dr Makirita Amani,
www.t.me/somavitabutanzania